

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA  
KAZI YA KIMISHENI ULMIWENGUNI KOTE

## NIPE MOYO WAKO

(Marko 10:17-23; Luka 18:18-24)


Jua lilikuwa limewaka sana katika sehemu hiyo ya mlima ambako kulijaa mawe wakati Yesu alikuwa akitembea kwenye barabara hizo zilizooja vumbi. Siku hiyo ilikuwa nedefu na wanafunzi hawa walikuwa wamechoka sana kutokana na kushughulikia makusanyiko ya watu ambao kila wakati waliwaandama.

Lakini kwa ghafla bwana mmoja ambaye alikuwa amevaa nguo za kitajiri akatokea huku akikimbia kwenye barabara hiyo kuwaelekeea. Na hapo akipunga pumzi kwa nguvu alisujudu mbele yake Yesu na kwa sauti ambayo ilijaa matarajio akamuuliza Yesu, "Mwalimu mwema, nifanye nini ili nipate kuurithi uzima wa milele?"

Yesu akasimama na kumtazama bwana huyu kwa huruma nyingi na akamjibu: "Wazijua amri, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako." Lakini huku moyo wake ukiwa umejaa ukweli kijana huyu akamwambia Yesu, "Haya yote nimeyashika tangu utoto wangu."

Yesu naye akageuza uso wake upande akiwa amejaa mawazo na kutafakari kuhusu mwanaume huyo ambaye alikuwa mbele zake. Alijua kwamba huyu alikuwa kiongozi, na kwamba alikuwa na utajiri mkubwa. Basi akaguzwa sana moyoni kuona kwamba kijana

huyu wa kuvutia alikuwa amejinyenyeka, na alikuwa na shauku ya kumpendeza Mungu. Ndipo (huku sauti yake ikiwa imejaa upendo) akamwambia, "Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo



*"Mtu kuwa na tabia nzuri  
na kudumisha nidhamu  
sio mambo yatoshayo  
kumfanya kupata uzima  
wa milele."*

vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate."

Uso wa kijana huyo ukakunjamana kwa maana maneno ya Yesu yalimfanya kufa

moyo, akasimama polepole huku moyoni akiwa amejaa masumbuko makubwa. Alipatwa na majonzi mengi kwa sababu alitaka sana kumfuata Bwana, lakini alikuwa na utajiri mwingu na basi hakuwa tayari kuuza mali yake. Basi huzuni kubwa ikionekana hata kwenye macho yake kijana huyu alitingiza kichwa chake na kuondoka kwa mwendo wa taratibu. Nayo macho ya Yesu yakaonekana kuja machozi alipomtaza kijana huyo akiondoka.

Hata ingawa Yesu alijua sifa nzuri za mwanaume huyo Yeye alitambua kwamba sifa hizo hazingemwezesha kijana huyo kuingia Mbinguni. Kuingia mbinguni kungemgharimu kijana huyo kutoa moyo wake na kumpenda Mungu kuliko kingine chote maishani mwake. Mungu alitaka kuwa mtawala wa shauku zote za kijana huyo. Naye Yesu alijua kwamba wakati utakuja ambapo upendo wa kijana huyo kwa mambo ya dunia kungevurugana na shauku lake la kumfuata Bwana. Basi Yesu alishughulikia msingi na maana ya kumfuata Yeye.

Mtu kuwa na tabia nzuri na kudumisha nidhamu sio mambo yatoshayo kumfanya mtu kupata uzima wa milele; pia mtu kuwa na na shauku ya mambo ya Mungu silo jambo ambalo linatosha. Inambidi mtu kujitoa mhanga kwa upendo wa kumfuata Bwana

(Endelea kwa ukurasa 2)

# MAMBO YENYE

# BIBLIA

## Inafundisha Kuhusu...

### Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

### Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, I Yoh. 4:7-21

### Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

### Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

### Uhuru Kutokana na Dhambi

I Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

### Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

### Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, I Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

### Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

### Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, I Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

### Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

### Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

### Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

### Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

### Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

### Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

### Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

### Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

### Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

### (Endelea kutoka ukurasa 1)

Yesu ili yeye aweze kurithi Mbingu. Tunaweza kuwa na shauku kwa Mungu, tunaweza pia kuwa na kiwango fulani cha upendo, tunaweza pia kuwa wake au waume wazuri (kwa watu amba tulioa), hata tunaweza kuwa wananchi wazuri, na pia kuwa majirani bora; lakini tunahitaji kuwa zaidi ya hayo.

Mungu anataka kwanza kabisa awe mtawala wa shauku zetu: "Mwanangu, nipe moyo wako; Macho yako yapendezwe na njia zangu" (Mithali 23:26). Maneno hayo yangali ndio kilio chake Mungu kwa mwanadamu— "Nipe moyo wako." Shauku zetu zote zinapokuwa kwake Mungu ndipo ambapo tunaweza kumpenda kwa mioyo yetu yote, nafsi zetu, mawazo yetu na nguvu zetu zote. Ni wakati ambapo Mungu amepata mioyo yetu ndipo anapata shauku zetu, wakati wetu, pesa zetu, ndoto zetu na hata mipango yetu. Wakati huo ndipo anakuwa nambari moja katika kila fani ya maisha yetu.

Watu wengi katika siku zetu huja kanisani huku wakitaka kujuu kuhusu Mbingu kama ambavyo kiongozi huyo tajiri alifanya. Lakini wengine wao huondoka kwa sababu hawako tayari kumpa Mungu shauku zao zote. Wengine nao washirika wa kanisa— huku wakiimba, wakiomba, wakifunza biblia na hata wakati mwingine wakihubiri; lakini wao huwa hawampatii Mungu "kitu hicho kimoja" ambacho hunabaki kuwa kizuiji cha upendo wao kwa Mungu.

Je, upendo wako uko wapi leo? Je, umebakisha kitu kimoja? Je, umejitolea mhanga kwa Mungu? Hebu mpe moyo wako. Chochote ambacho utahitaji kuachilia basi kiachilie ili umfuate Bwana Yesu nawe utorialiwa kwa zawadi kuu katika maisha haya na hata katika siku zizajo.

—mws

### UKWELI WA INJILI

Gazeti la 'Ukweli wa Injili' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia amba umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaotewa na utakaso wa Yesu Kristo; amba hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamiletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinasi na wa upendo amba msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

### UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anayyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) ili uagize jalida hili kuititia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebujisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine amba wangependza kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

### WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kuititia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

The Gospel Truth, PO Box 2042, Nixa, MO 65714 USA

[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

# Tahariri



*Haleluya. Nampenda BWANA kwa kuwa anaisikiliza Sauti yangu na dua zangu. Kwa maana amenitegea sikio lake, Kwa hiyo nitamwita siku zangu zote —Zaburi 116:1-2*

Nikiwa mtoto mdogo niliutoa moyo wangu kwa Mungu na kujisalimisha kwa utunzi wake. Mimi ninakumbuka sana jinsi nilivyodondokwa na machozi kwa vile ambavyo Roho Mtakatifu alifanya kazi yake ya kunihakikishia moyoni mwangu. Hapo katika chumba cha nyuma katika Shule ya Jumapili mama yangu aliomba nami ili Yesu aingie moyoni mwangu. Hata ingawa sikuwa nimejingiza sana dhambini nilihitaji neema ile ya wokovu wa Mungu ambayo humwokoa mwanadamu iingie katika maisha yangu kama jinsi ambavyo mshiriki wa madawa ya kulevy hata mlevi wa pombe anahitaji. Na nilipokuwa nikikua na kukomaa mimi nilipitia na “uchungu wa kukua kiroho” hata wakati mwininge nikakosa kufikia malengo ya maisha ya Kikristo—kama ambavyo hutokea kwa watu wengi amba wanaokoka wakiwa wangali wadogo. Lakini kamwe sikuwahi kupoteza shauku langu la kumtumikia Mungu, hata ingawa nilifanya safari nyngi madhabahuni ili kuombewa kuokoka tena. Hadi leo mimi ninamshukuru Mungu kwa ajili ya uaminifu wa Roho wake. Kama wimbo unavyosema, “Roho ndiye aliyeniongoza hadi mahali nilipo sasa.” Mimi nilikuwa (na ningali) na shauku kubwa sana ya kuwepo na uwepo wa Mungu maishani maishani mwangu kila siku, kwa maana nikifuata njia zangu mwenyewe nitapotea.

Mimi nampenda Bwana na ninatilia umuhimu swala la uwepo wake maishani mwangu hata kuliko uhai wangu mwenyewe. Mungu amekuwa mwaminifu kusikia sauti yangu na kujibu maombi yangu. Yeye ameponya mwili wangu na akaniokoa kutoka mautini, na pia amenipatia familia ya ajabu, na kukutana na mahitaji yangu ya kila siki; zaidi ya yote Yeye aliniokoa kutokana na minyororo na utumwa wa dhambi. Amenipatia amani yake na uwepo wa Roho wake Mtakatifu. Kwa kweli ninayo mengi ya kumshukuru Mungu. Hata ingawa wewe unakumbana na majoribu na masumbufo ya aina nyngi kama unampenda Bwana maishani mwako una hazina kuu zaidi kuliko ingine ulimwenguni mote. Tolea hili la *Ukweli wa Injili* linatilia umuhimu amri ambayo ni kuu zaidi na mafundisho ambayo ni makuu zaidi katika Biblia, maanake—Upendo.

Unapokazana na mwaka huu mpya uwe na uhakika kwamba Mungu ataendelea kuwa mwaminifu kwako. Kama jinsi ambavyo amekutana na mahitaji yako hapo mbeleni na kukuwezesha kuititia mabonde na hata motoni ndivyo ambavyo atakuwa nawe mwaka huu. Ewe msafiri pamoja na Yesu, endelea kuwa mwaminifu na uendelee kumtumaini Bwana wako. Ushindi mpya wakungoja na ukiendelea kushikamana naye Yesu siku moja utatembea naye Mbinguni.

Ombi langu ni kwamba toleo la jalida la *Ukweli wa Injili* litaendelea kuwa na himizo na msaada mkuu kwa kila msomi hapa kwetu nyumbani na hata katika nchi za kigeni. Kama gazeti hili limekuwa la msaada kwako sisi tutapata kujengwa katika kazi hii ikiwa utaweza kutuandikia kuhusiana na swala hilo. Basi jisikie huru kuniandikia kwa njia ya moja kwa moja kuititia kwa barua pepe:

[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org).

Basi ni ombi letu kwamba Mungu atakubariki na kukupatia mwaka wa ajabu kuititia kwa uwepo wake. Ninaomba kwamba tutembee katika mwanga na utakatifu wa Neno lake Mungu ili tuweze kudumu katika amani.

—Michael W. Smith

Januari 2013.

mengi kwa  
MTANDAO

*Tutembelee katika*

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

*ili uagize na uweze*

*kupata toleo za*

*hapo mbeleni.*

Ukurasa wa 3



## JINSI YA KUTILIA NGUVU UPENDO WAKO KWA MUNGU

### TUBU

Kubali kwamba umekuwa mlegevu na kwamba umepoteza ari yako na bidii kwa Mungu. Tubu na umwombe Mungu msamaha na kwamba akurudishe mahali ambapo ulikuwa hapo mbeleni kwa mambo yako ya kiroho.

### MTAFUTE MUNGU

Anza kujifunza maandiko tena kwa bidii. Mwombe Mungu akurudishie shauku ya kuupenda ukweli na haki.

### KUWA MTIIFU

Jitenge kutokana na mambo ambayo yatakuvuta mbali na Mungu na kukupeleka mbali na makusudio yake maishani mwako. Utiiufu ni jambo ambalo hutokana na mtu kufanya uchaguzi wa wazi wa kumpenda Mungu zaidi ya mambo mengine yote.

### USIPUUZE USHIRIKA

Usiache kutilia maanani swala la kuhudhuria ibada. Andaa moyo wako na uweke kando kila jambo ambalo linakusumbua wakati ambapo umeingia nyumbani mwake Mungu.

### WATUMIKIE WENGINE

Usiuruhusu ubinafsi ufanye uwe na uvuvi wa kiroho. Mwombe Mungu akuonyeshe jinsi utakavyomtumikia kwa kuwatumikia wale amba wako karibu nawe.

### KUWA NA FURAHA YA WOKOVU

Dumu ukiwa na moyo amba una shukrani kwa ajili ya baraka zake Mungu. Kila siku mwonyeshe Mungu upendo wako (kwake) kwa mambo yote unayofanya.

# MAFUNZO YA BIBLIA

## SOMO: UHUSIANO UNAOONGOZWA NA

**Somo la Biblia:** *Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake. Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu.*

– 1 Yohana 4:16-70

**Maana ya upendo:** Kuvutiwa na mtu, kumtakia mema, kumfanya mema, kushikamana na mtu. Tendo la mtu analochagua kufanya.

### I. Mawazo ya Mungu kwa Mwanadamu

- A. Yeremia 31:3 Kuvutiwa na fadhili zake.
- B. Yeremia 29:11-13 Mawazo ya amani.

### II. Shauku la Mungu la Kuwa na Uhusiano na Mwanadamu

- A. Mwanzo 3:8-9 Mungu alikuwa na shauku la ushirika.
- B. Ufunuo 3:20 Tazama nasimama mlangoni.
- C. 2 Wakorintho 5:17-18 Kupatanishwa na Mungu.

### III. Mungu Anapenda Nani?

- A. Yohana 3:16 Ulimwengu.
- B. Warumi 5:8 Watu wenye dhambi.
- C. Waefeso 5:25 Kanisa.

### IV. Dhihirisho la Upendo wa Mungu

- A. 1 Yohana 4:9-10 Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee.
- B. 1 Yohana 3:1,16 Tazameni ni pendo la namna gani.

### V. Upendo Ndio Amri Kuu Zaidi

- A. Kumbukumbu 10:12 Upendo umeamriwa.
- B. Mathayo 22:36-38 Mpende Bwana wako.
- C. 1 Wakorintho 13:1-3 Bila upendo.

### VI. Upendo ni Kipawa cha Mungu

- A. 1 Yohana 4:7-8 Upendo unatokana na Mungu.
- B. Warumi 5:5 Upendo unatolewa na Roho Mtakatifu.

### VII. Upendo Ni kwa Matendo

- A. 1 Yohana 3:18 Tupendane kwa matendo na kweli.
- B. Mathayo 15:8 Wengine huniheshimu kwa mdomo.

### VIII. Jinsi Upendo Wetu kwa Mungu

#### Unavyojidhahirisha

- A. Yohana 14:15, 23-24 Atadumisha maneno yangu.
- B. 1 Yohana 5:3 Atadumisha amri zake.
- C. 1 Yohana 4:20-21 Twawapenda ndugu.

### IX. Haiwezekani Kumpenda Mungu na Ulimwengu

- A. Mathayo 6:24 Huwezi kutumikia mabwana wawili.
- B. 1 Yohana 2:15-17 Usiupende ulimwengu.
- C. Kumbukumbu 13:3 Bwana hujaribu upendo wetu.

### X. Sifa za Upendo wa Kweli

- A. 2 Wakorintho 6:6 Hauna unafiki.
- B. 2 Wakorintho 8:8 Wenye unyoofu.
- C. 1 Timotheo 1:5 Unaotokana na moyo safi.

### XI. Ukamilifu Unaotokana na Upendo

- A. Waefeso 3:17-19 Utimilifu wa Mungu.
- B. Yohana 15:10-11 Ili furaha yenu itimizwe.

### XII. Nguvu za Upendo

- A. 1 Yohana 4:18 Upendo ulio kamili hutupa hofu nje.
- B. 2 Wakorintho 5:14-15 Upendo hubidisha.

### XIII. Ni Nini Hutenganisha Mwanadamu na Upendo wa Mungu?

- A. Warumi 8:35 Ni nani atatutenganisha?
- B. Yohana 14:23-24 Kutofuata amri.

### XIV. Kupoteza Upendo

- A. Mathayo 24:12 Upendo utakuwa baridi.
- B. Ufunuo 2:4 Kuacha upendo wa kwanza.
- C. Ufunuo 3:15-17 Si moto si baridi.

### XV. Kipawa kwa Wale Wampendao Mungu

- A. Yakobo 2:5 Warithi wa ufalme.
- B. 2 Timotheo 4:7-8 Taji la haki.

# SHAUKU KUBWA YA MUNGU

Nakala ya kuandamana na Mafunzo ya Biblia

## MUNGU AMTAFUTA MWANADAMU

Tangu kuumbwa kwa ulimwengu Mungu amekuwa na shauku ya kuwa na uhusiana na mwanadamu. Tunasoma jinsi Mungu alitembea katika Shamba la Edeni wakati wa kupunga hewa ya mchana huku akiwa na shauku la kuwa na ushirika na Adamu na Hawa (Mwanzo 3:8-9). Ingawa Biblia ni historia na kitabu cha thiolojia kusema kweli biblia ni nakala ya shauku la Mungu na juhudhi zake za kutafuta uhusiano wa upendo na wanadamu.

## DHAMBI YAVUNJA UHUSIANO NA MUNGU

Mungu aliumba wanadamu na shauku lake kuu ni kuwa na uhusiano na viumbe wake—sio kwa njia ya kushurutishwa bali kwa upendo. Adamu na Hawa walikosa kumtii Mungu na dhambi yao ikawatenganisha na uhusiano wa karibu ambao walikuwa nao na Mungu hapo mbeleni. Daima dhambi huvunja uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu. Lakini Mungu hakurusu utengano ulioletwa na dhambi, ukosefu wa utakatifu, na hukumu ya kifo iliyo kuu yetu kuendelea kututenganisha naye.



## MUNGU ALIMTUMA MWANAWE ILI TUPATANISHWE NAYE

Mungu alitupenda sana hata akamtuma Mwanawe wa pekee duniani ili tuweze kuokolewa (Yohana 3:16). Msukumo ambao Mungu alikuwa nao ulikuwa ni wa upendo na upendo huo ungaliko hawa wakati wa sasa: "Bwana alinitokea zamani, akisema, Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu" (Yeremia 31:3).

## MATENDO YOTE YA MUNGU HUTOKANA NA UPENDO

"Mungu ni upendo"(1 Yohana 4:8) na hiyo ndio nguzo ya mahusiano yake na wanadamu. Wengine humwona Mungu kama Mungu wa kufanyisha watu kazi ya sulubu—ambaye ana matakwa mengi na ambaye ni vigumu kumpendeza. Lakini picha hii inamwakilisha Shetani, haimwakilishi Mungu. Mungu ni Mungu wa upendo ambaye hujali kuhusu

mambo yote ambayo huadhire maisha yetu. Yeye anajaribu kumfikia kila mwanadamu kwa upendo haijalishi hali yake. Kamwe sisi hatustahili upendo wa Mungu na hakuna chochote ambacho tumefanya cha kustahili upendo huo. "Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikuwa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8).

## UPENDO UKIPATANA NA UPENDO HUWA UPENDO ULIOKAMILIKA

Kama upendo haupewi upendo huwa basi haujakamiika. Mungu anatupenda lakini upendo huo haukamiliki hadi hapo tunapompenda bila kujibakishia chochote na kwa moyo wetu wote. Mwanasheria mmoja alimuuliza Yesu, "Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.

Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza." Mafundisho mengine yote huwa bure iwapo msingi wake sio sheria hii ya kwanza na iliyo kuu zaidi. Watu wengi humtumikia Mungu kuto kana na woga au kwa kujitolea kwa kanisa au kwa thiolojia fulani. Lakini uhusiano wa upendo huwa wenye kina zaidi na utajiri mkubwa. Uhusiano wa upendo huleta utoshelevu wa kweli kwa maana sasa uhusiano huwa umekamilika. Hii ndiyo chanzo cha amani ya kweli na furaha ya kumtumikia Mungu.

## UPENDO WA KWELI HAUPATIKANI KWA NJIA YA MABAVU

Kulikuwa na jamaa mmoja ambaye angemfungia mkewe kwa nyororo jikoni mwao kila siku alipokuwa akitoka kwenda kazini. Yeye alikuwa na hofu kwamba mkewe angemwacha na asirudi. Uhusiano wao ulikuwa wa uongo na utumwa. Ingekuwa afadhali zaidi kama mume

(Endelea kwa ukurasa 6)

(Endelea kutoka ukurasa 5)

angeondoka kwenda kazini huku akifahamu kwamba mkewe angekuwa tu hapo nyumbani atakaporudi kwa sababu mke huyo alimpenda. Huu ndio uhusiano ambaao Mungu anatamani—uhusiano ambaao mtu hashurutishwi kuishi kwa utakatifu lakini ambaao mtu anaishi kwa utakatifu kutokana na moyo wake wa upendo. Nguvu za upendo ndizo husukuma watoto wa kweli wa Mungu kuishi maisha matakatifu (2 Wakorintho 5:14).

### **USHAHIDI WA UPENDO WETU NI UTIIFU WETU**

Watu wengi humkaribia Mungu kwa vinywa vyao na kumtukuza kwa midomo yao huku miyo yao ikiwa mbali naye (Mathayo 15:8). Lakini upendo wa kweli haudhihiriki kwa maneno tunayonena bali kwa tabia za maisha yetu. “Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno



langu” (Yohana 14:23). Huu ndio ushahidi wa kweli wa upendo katika ulimwengu ambaao wengi humkiri Kristo lakini ni wachache ambaao hutii Neno la Mungu. Mahali ambako hamna utiifu hapana upendo. Hakuna chochote ambacho kinaweza kututenganisha na upendo wa Mungu (Warumi 8:35) isipokuwa kutokutii kwetu (Yohana 14:23-24).

### **HAKUNA UPENDO MWINGINE ISIPOKUWA “UPENDO WA KWANZA”**

“Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili” (Mathayo 6:24). Hakuna nafasi katika uhusiano na Mungu wa mtu kufuata ulimwengu wenyewe dhambi na wakati huo huo

kumfuata Mungu. Mtu akipenda ulimwengu upendo wa Baba haumo ndani yake (1 Yohana 2:15-17).

### **UPENDO HUFANYA MTU KUJITOA MHANGA**

Wakati watu wawili wanapendana kwa kweli wao huwa tayari kujinyima wakati na uwezo wao ili wawe pamoja. Shauku yao kubwa huwa ni mmoja kumpendeza mwininge. Jambo hili huwa la kweli hata kwa upendo wa kweli kwa Mungu utokao moyoni mwa mtu. Upendo humfanya mtu kumwabudu Mungu kwa hiari yake mwenyewe na kumtumikia. Basi utiifu unakuwa si kazi ngumu ya sulubu bali huwa ni dhihirisho la upendo. Upendo huleta furaha, kutoshereka, na nguvu katika utumishi kwa Bwana.

### **APENDAYE MUNGU HUPENDA NDUGU YAKE**

Watu wanapopata ujuzi wa upendo wa Mungu upendo wak humwagwa miyononi mwao kupitia kwa Roho Mtakatifu (Warumi 5:5). Uhusiano huo huonekana sio tu kupitia kwa mtu kuwa mtiifu kwa Mungu bali pia kwa upendo ambaao mtu huonyesha ndugu zake kanisani. Kwa maana mtu asipopenda ndugu yake basi upendo wa Mungu haumo ndani yake (1 Yohana 4:20-21).

### **UPENDO MKAMILIFU HUTUHAKIKISHIA UZIMA WA MILELE**

Sio tu kwamba uhusiana wa upendo na Mungu hutuletea amani na uhusiano wa karibu na Mungu bali pia unatuuhakikishia uzima wa milele. “Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake (1 Timotheo 4:8).

### **SHAUKE KUU LA MUNGU NI KUWA NA UHUSIANO NAWE**

Shauku kuu la Mungu ni wewe kuwa na uhusiana na urafiki wa karibu naye. Mungu angetaka kuwa sehemu ya maisha yako. Yeye ana shauku kwamba utatumia wakati wako na Yeye na pia kwamba utawasiliana na Yeye. Kuna ushirikia wa karibu na wa ajabu ambaao unapatikana katika uhusiano kama huo. Uhusiano na Mungu ambaao msingi wake ni upendo utapatia maisha yako maana na kusudi la kuishi.

—mws.

# MASWALI na MAJIBU

**SWALI:** Je, ni nini maana ya mtu kupoteza upendo wa kwanza?

**JIBU:** Swahili hili linaambatana na andiko la Ufunuo 2:4 ambalo linasema: "Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza." Roho wa Mungu alikuwa akizungumza kuhusu kusanyiko la Efeso.

Zingatia kwamba kusanyiko hili lilikuwa limesimama wima dhidi ya uovu na walikuwa wakifanya mambo mengi yaliyokuwa mazuri na ya haki. Ingawa walikuwa watiifu kwa mambo ya thiolojia na mafunzo ya kanisa Waefeso walikuwa wamepoteza uhusiano wa upendo uliowaambatanisha na Mungu ambao walikuwa nao hapo mbeleni. Nakala ya mafafanuzi cha JFB inasema: "Joto lao la upendo lilikuwa limeondoka na badala yake wakapatwa na maisha ya kushikilia mafundisho ya Kikristo kwa nguvu na ambayo hayakuwa na uhai."

Wakati mwangi Maandiko hulinganisha uhusiano kati ya mwanadamu na Kristo kuwa kama ule wa kati ya bwana na mkewe. Hebu fikiria kuhusu wapenzi ambao walioa majuzi na ambao wanapendana sana na kujitolea mmoja kwa mwagine kwa uhusiano ulio hai. Wao hutaka kutumia wakati mwangi pamoja na kujinyima mambo mengi mmoja kwa ajili ya yule mwagine. Ndoa yao huwa na moto sana na pia uhai mwangi.

Lakini kama inavyokuwa wakati mwangi kwenye ulimwengu huu wenye dhambi wapendanaao hypoteza ule upendo wao wa mmoja kwa mwagine na ndoa yao inakosa uhai. Wao huanza kuishi tu kwenye nyumba moja lakini joto la

upendo wao huwa limetokomea. Na mambo pia huwa hivyo kwa watu wengi katika uhusiano wao na Mungu. Waokovu wapya huwa na wakati mzuri wakiwa katika hali hiyo ya kujihisi wamesamehewa dhambi zao na wako kwenye maisha yaliyoja amani na neema. Lakini ikiwa uhusiano huo haudumishwi mtu huyo anaweza aidha kuirudia dhambi ama kuendelea kufanya mambo "ya haki" lakini bila ukakamavu wa upendo huo wa kwanza.

Wale ambao wamepoteza upendo wa kwanza wameamuriwa kutubu. Kunao watu wengi na makusanyiko mengi ambayo wamesimama wima dhidi ya

Kikristo yenyeye uchovu mwangi ya kuwa na msimamo dhabiti kwa mafundisho ya Kikristo lakini bila upendo wa kupatia maisha hayo uhai. Uhusiano huchukuwa wakati wa mtu. Pia unahitaji kulindwa dhidi ya mambo ambayo yanaweza kuingilia kati.

"Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapo" (Mathayo 24:12). Wengi wamepoteza upendo wao wa kwanza kwa maana wametoa upendo wao kwa mambo ya ulimwengu huu huku wakidumisha msimamo ambao kimsingi unaambatana na mafundisho ya Kikristo. Mungu basi anakuwa na wa kiwango cha pili kwa upendo wao au hata anakuwa ni wa kiwango cha chini zaidi. Wakati wao, uwezo wao, umakini wao, na mvuto wa upendo wao unakuwa kwa mambo mengine.

Jambo hili huleta uvivu kwa maisha ya mtu kumwishia Mungu na kunakuwa na ukosefu wa bidii ya kueneza injili. Kunakuwa tu na aina ya utauwa. Basi ni jambo muhimu kwetu kuchunguza tena maisha yetu ili kuhakikisha kwamba maisha yetu na bidii yetu ili kuhakikisha kwamba hatupotezi upendo wa kwanza.

Kama ambavyo mke na mume wanahitaji kuwasiliana na kutumia wakati pamoja ili kudumisha upendo wao ukiwa wenye nguvu ndivyo hivyo ilivyo kwa Mungu. Ni jambo muhimu kwetu ni kufanya bidii kudumisha "upendo wa kwanza" kwa kusoma Neno la Mungu, kuomba, kudumisha mahusiano, na kumweka Mungu mwanzo katika maamuzi yote tunayofanya. Zaidi ya yote tunahitaji kuufanya upendo kuwa ndio msukumo wa huduma yetu na sababu yetu ya kufanya mambo yafaayo.

Ni katika ujuzi huo wa upendo wa kwanza ndipo utakapopata bidii ya kushiriki injili na upako wa maisha ya kila siku. Upendo huo hufanya mafundisho ya Kikristo kuwa hai na kutoa sababu na furaha ya maisha.

—mws



*"Wengi wamepoteza  
upendo wao wa kwanza . . .  
  
Wakati wao, uwezo wao,  
umakini wao,  
na mvuto wa upendo wao unaku-  
wa kwa mambo mengine . . .  
Mungu basi anakuwa na wa  
kiwango cha pili kwa upendo  
wao au hata anakuwa ni wa  
kiwango cha chini zaidi."*

uovu lakini wamepoteza moto wa upendo ambao ulikuwa ukiwaka hapo mbeleni. Wao wamepoteza kile kitu ambacho Mungu alitaka wawe nacho toka mwanzo—uhusiano wa upendo.

Upendo mkuu kwa Mungu ndio huleta joto katika huduma ambayo mtu anamfanya Mungu. Basi tusianguke kwenye mtego wa kuwa na maisha ya



## Je, Wajua?

- Yehova (Yahweh – Kiebrania) ni jina la kibinaksi la Mungu katika Maandiko. Mungu yule ambaye ana uhai wake wa kibinaksi, asiyebadilika, wa milele, muumbaji na Bwana wa yote.
- Yesu ni jina lenye maana ya “Mwokozi.”
- Imanueli ni jina lenye maana ya “Mungu pamoja nasi.”
- Masihi nalo linatokana na Kiebrania na maana yake ni “kupakwa mafuta.”
- Kristo ni neno la Kiyunani lenye maana ya “aliyepakwa mafua.” Jina hili lina maana moja na Masihi.
- Alfa na Omega ni herufi za kwanza na za mwisho za alfabeti ya Kiyunani. Maana yake ni kumwakilisha Yesu kama “mwanzo na mwisho, maana yake ni wa kwanza na wa mwisho.”



## Sio kwa Ufasaha wa Maneno

### Anwani

The Gospel Truth  
P.O. Box 2042  
Nixa, MO 65714  
USA  
Email:  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

### UTAKATIFU KWA BWANA

*Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa. Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu. —1 Wakorintho 2:1-5*

Jumapili moja mhubiri Charles Haddon Spurgeon ambaye anajulikana kama “mhubiri wa wahubiri” alijihisi kwamba amehubiri kwa njia dhaifu sana hivi kwamba akajionea aibu. Alipokuwa akiondoka kutoka mle kanisana mwake lililokuwa katika mji wa London na ambalo lilijulikana kama Metropolitan Tabernacle yeye aliduwazwa na swalii kama kwamba kutakuwa na jambo lolote nzuri ambalo lingetokana na ujumbe kama huo wake. Alipofika nyumbani akapiga magoti na kuomba, “Ewe Bwana Mungu, waweza kufanya kitu bila kuwa na chochote. Naomba ukaubariki ujumbe huo wangu ambao ni hafifu sana.”



Kwa muda wa miezi kadhaa iliyofuata watu 41 wakasema waliamua kumwamini Kristo kama mwokozi kutopteka na ujumbe huo “dhaifu.” Katika Jumapili iliyofuata na ili kufuta “makosa” yake Spurgen aliandaan ujumbe “kemkem” lakini ng’o hakuna mtu aliyeokoka.

Ujuzi ambao Spurgeon alipata unatilia mkazo masomo mawili muhimu kwa watu wote wamtumikiao Bwana. Kwanza kabisa tunahitaji baraka za Mungu kwa juhudii zetu zote. Sulemani alisema katika Zaburi 127:1, “BWANA asipojenga nyumba waijengao wanafanya kazi bure.” Pili, udhaifu wetu huwa nafasi kwa Mungu kudhihirisha nguvu zake. Mtume Paulo akasema, “Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na matusi, na matatizo, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu” (2 Wakorintho 12:10).

*Mkate Wetu wa Kila Siku, Mei 18, 1992.*